



# MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA YA KUTOA HUDUMA YA KUANDAA MPANGO KAZI WA ZIADA WA UHAMISHAJI WA WATU NA MAKAZI PAMOJA NA MPANGO WA UREJESHAJI WA UWEZO WA KUJIKIMU KWA AJILI YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) KUMBUKUMBU NA: 0010006870

TOTAL East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, kampuni ya kimataifa ya nishati, inaalika makampuni/taasisi yenye utaalumu na uzoefu katika Uhamishaji wa Watu na Makazi Pamoja na Urejeshaji wa Uwezo wa Kujikimu kutuma nia ya kutoa huduma katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha Mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta hayo katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni karibia kilomita 1,443, kati hizo kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Ardhi imeshatwaliwa katika rasi ya Chongoleani kwa ajili ya ujezi wa kitua cha kuhifadhia mafuta kilicho pembezoni mwa bahari na kugusa jamii ambazo zinategemea ardhi pamoja na bahari ili kuweza kujikimu.

## MAELEZO MAFUPI YA MAWANDA YA HUDUMA:

Kampuni inahitaji huduma kutoka kwa makampuni/taasisi yaliyobobea/iliyobobea katika Uhamishaji wa Watu na Makazi Pamoja na Urejeshaji wa uwezo wa kujikimu kwa lengo la:

- Kuandaa Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP) wa ziada kwa ajili ya Waguswa wa Mradi waliopo katika jamii inayoishi kwenye Rasi ya Chongoleani.
- Kufanya tathmini ya uwezo wa kujikimu (katika matumizi ya ardhi Pamoja na bahari) katika jamii.
- Kuandaa Mpango wa Urejeshaji wa Uwezo wa Kujikimu (LRP) kwa ajili ya Jamii ya Rasi ya Chongoleani iliyoguswa na Mradi.

## VIGezo MUHIMU:

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa kuandaa Mipango Kazi ya Uhamishaji wa Watu na Makazi Pamoja na Mipango ya Urejeshaji wa Uwezo wa Kujikimu katika miradi ya viwanda barani Afrika.
- Uthibitisho wa uzoefu wa kusanifu mipango ya uhamishaji wa watu na makazi pamoja na mipango ya urejeshaji uwezo wa kujikimu katika miradi mikubwa ya ujenzi inayodhaminiwa.
- Afisa anayependekezwa pamoja na wataalam wa maswala ya ardhi na uwezo wa kujikimu katika matumizi ya ardhi na bahari pamoja na uzoefu wao katika kutoa huduma kwenye eneo husika.
- Uthibitisho wa usajili wa watekelezaji wa ngazi za juu katika taasisi za kitaaluma za Kitanzania au shirikisho.
- Usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma wa Ndani ya EWURA (LSSP) katika kipindi cha kuwasilisha majibu ya nia kwa ombi hili yanahimizwa.

Makampuni zenye nia, uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: [robin.schroh@external.totalenergies.com](mailto:robin.schroh@external.totalenergies.com) (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00 jioni** Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **25 Agosti 2021**.

**Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).**